# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA HAMSINI

**20 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA HAMSINI - TAREHE 20 JUNI, 2025

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**636 MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha lami kuunganisha kipande cha Mbutu na Igunga Mjini.

**637 MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mpalanga – Bahi.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**638 MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi nchini.

**639 MHESHIMIWA BERNADETA KASABAGO MUSHASHU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Biashara ya kununua na kuuza *Carbon* imeinufaishaje Tanzania.

**WIZARA YA NISHATI:**

**640 MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itafanya juhudi za makusudi kupeleka umeme kwenye maeneo ya Wachimbaji Wadogo Wilayani Chunya.

**641 MHESHIMIWA LUCY JOHN SABU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwa na Sera rafiki ya nishati ya umeme kwa Vijana wanaojihusisha na uzalishaji kwenye Viwanda vidogo vidogo.

**WIZARA YA MAJI:**

**642 MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga Mradi wa Maji wa Kyerwa, Nyakatuntu na Kamuli – Kyerwa.

**643 MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa Maji katika Mji wa Geita uliosainiwa Mwaka 2022 utakamilika na kuanza kutoa huduma ikizingatiwa kuwa mradi huu ni wa muda mrefu.

**644 MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini kazi ya kuleta maji ya Mto Momba katika Miji ya Tunduma, Mlowo na Vwawa itaanza.

**645 MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini maji ya DAWASA yatasambazwa Jimbo la Mbagala Mitaa ya Majimatitu, Machinjioni, Serenge, Changanyikeni, Vikunai, Kongowe na Masaki.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**646 MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Maziwa Kijiji cha Likiushin Mnadani - Arumeru Magharibi.

## WIZARA YA UJENZI:

**647 MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini lami itawekwa kwenye Barabara ya kutoka Mroyo hadi Ndungu Wilayani Same.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**20 JUNI, 2025** **KATIBU WA BUNGE**